Eastern Africa Journal of Kiswahili

[ISSN 2958-1036]
Volume: 05 Issue: 01 | August-2026

EAJK

Mchango wa Fasihi ya Watoto katika Uwasilishaji wa Hisia

Authors
Leah Njeri Njuguna [1]; Joseph Maitaria [2]; Peter Kinyanjui [3]
Main author's email: Leahnjuguna31@gmail.com

(1.2.3) Karatina University, Kenya.

Cite this article in APA
Njuguna, L. N., Maitaria, J., & Kinyanjui, P. (2026). Mchango wa fasihi ya watoto katika uwasilishaji wa hisia. *Eastern Africa journal of Kiswahili, 5*(1), 134-143. https://doi.org/10.51317/eajk.v5i1.1132

OPEN ACCESS
A publication of Editon Consortium Publishing (online)

Article history
Received: 2026-06-16
Accepted: 2026-07-18
Published: 2026-08-31

Scan this QR to read the paper online

Copyright: ©2026 by the author(s). This article is an Open Access article distributed under the terms and conditions of the Creative Commons Attribution-NonCommercial-ShareAlike 4.0 International License (CC BY-NC-SA 4.0).

Ikisiri

Makala hii ililenga kubainisha jinsi hisia za watoto zinavyowasilishwa katika fasihi ya watoto ya Kiswahili, kwa kuzingatia mchango wa mazingira ya kifamilia na kijamii katika kuathiri hisia hizo. Fasihi ya watoto ni nyenzo muhimu ya kuakisi hali halisi ya maisha ya watoto. Hususan hisia wanazopitia katika mazingira yao ya kifamilia na kijamii. Mtazamo wa awali ulichukulia fasihi ya watoto kama chombo cha burudani na ufundishaji wa lugha. Fasihi ya kisasa inawakilisha kwa upana ulimwengu wa mtoto. Fasihi inaweka wazi changamoto, uzoefu na hisia mbalimbali katika maisha ya watoto. Kuna haja ya kuchunguza hisia zinazotokana na mazingira ya familia. Makala haya yalilenga kutathmini jinsi hisia za watoto zilivyowasilishwa katika fasihi ya watoto ya Kiswahili. Uchambuzi uliongozwa na Nadharia ya Uhalisia, ambayo ilisisitiza uwasilishaji wa maisha jinsi yalivyokuwa bila kupiga chuku. Kupitia nadharia hiyo, ilibainika kuwa waandishi waliwasawiri watoto wakipitia hisia kama vile furaha, huzuni, hofu, hasira, upweke, upendo na wasiwasi. Hisia hizo zilichochewa na mazingira ya kifamilia, uhusiano na wazazi, hali ya kiuchumi, migogoro ya ndoa, mazingira ya shule na mwingiliano wao na jamii. Utafiti huu ulitumia mbinu ya kimaelezo na uchanganuzi wa matini. Data ilikusanywa kutoka kwa novela zifuatazo: *Ahaa! Roda*, *Mshale wa Matumaini* na *Siri ya Baba Yangu*. Novela hizi ziliteuliwa kimakusudi. Uchambuzi ulionyesha kuwa familia ni mazingira muhimu katika kujenga na kuathiri ustawi wa kihisia wa watoto. Makala haya yalihitimisha kuwa fasihi ya watoto ya kisasa imechangia kuhalalisha hisia za watoto. Fasihi inaelimisha watoto kuhusu hali zao za kisaikolojia. Kwa msingi huo, makala haya yalipendekeza kuwa hisia za watoto zitambuliwe na zipewe uzito katika familia, shule na jamii ili kuimarisha ustawi wao wa kihisia, kijamii na kisaikolojia.

Maneno muhimu: Familia, fasihi ya watoto, Hisia, mtoto.

UTANGULIZI

Tafiti nyingi za fasihi ya watoto zimeshughulikia masuala ya maudhui kama vile malezi, elimu, haki za watoto na maadili. Tafiti zingine zimeonyesha umuhimu wa fasihi kama bibliotherapia katika ukuaji wa mtoto. Usawiri wa hisia za watoto katika fasihi ya watoto ya Kiswahili ni suala ambalo linahitaji utafiti zaidi. Hisia hizo huibuliwa na mazingira tofauti. Zipo hisia zinazozuka kutokana na mazingira ya familia. Kwa kuzingatia pengo hilo, makala haya yalichunguza namna fasihi ya watoto ya Kiswahili ilivyowasilisha hisia za watoto. Makala haya yalitathmini jinsi waandishi walivyowasawiri watoto waliokabiliwa na mazingira magumu ya kifamilia na jinsi hisia zao zilivyoathirika. Mtafiti alichunguza jinsi hisia za watoto zilivyojitokeza katika matini. Uchambuzi ulijengwa na mifano kutoka novela ya *Ahaa! Roda* (Nyambeka, 2017), *Mshale wa Matumaini* (Habwe, 2022) na *Siri ya Baba Yangu* (Mutuku, 2017).

MAPITIO YA MAANDISHI

Fasihi ya watoto imepitia mageuzi makubwa kutoka chombo cha burudani na maadili hadi kuwa nyenzo muhimu ya kuwasilisha tajriba halisi za watoto. Mitazamo ya awali iliitazama fasihi ya watoto kama kazi iliyoandikwa kwa madhumuni ya kuwaburudisha watoto na kuwafundisha maadili mema pamoja na matumizi ya lugha. Lukens (2007) alieleza kuwa fasihi ya watoto ilikuwa na lengo la kuwapa watoto furaha na starehe. Kulingana naye vipengele vya fasihi vilikuwa na matukio ya kusisimua yaliyowafanya watoto wafurahie.

Fasihi ya watoto imeendelea kupanuka. Matini za watoto zinatumiwa kuwasilisha changamoto halisi zinazowakabili katika maisha yao ya kila siku. Wataalamu kama vile Nodelman (2008) na Nyaga (2022) wakieleza kuwa fasihi ya watoto ni kazi inayosawiri ulimwengu na mahitaji ya mtoto. Ulimwengu wa mtoto unahusu maisha na hisia zake. Kwa mujibu wa Wamitila (2010), fasihi ya watoto inaweza kufafanuliwa kwa kuzingatia hadhira inayolengwa au maudhui yanayowahusu watoto. Mtazamo huu unaonyesha kuwa fasihi ya watoto si matini inayokusudiwa kuburudisha pekee, bali inaweza kuwasilisha tajriba inayogusa maisha ya watoto. Mawazo ya Bakize (2014) na Wamitila (2010) yakioana kuhusu watoto kutafakari maisha yao kwa kutumia tajriba za wahusika katika kazi za fasihi. Bakize (2014) anaendeleza hoja hii kwa kueleza kuwa fasihi ya watoto imejijengea utambulisho wake kama tawi muhimu la fasihi linaloweza kuchunguzwa kwa misingi yake yenyewe. Kwa mtazamo huo, watoto hawaonekani tena kama wapokezi wa hadithi pekee bali kama wahusika wenye sauti, hisia na tajriba zinazostahili kupewa nafasi katika fasihi. Utafiti huu ulitumia maoni yao kueleza fasihi ya watoto kama nyenzo muhimu ya kuelewa ulimwengu wa kihisia wa mtoto.

Hisia ni sehemu muhimu ya maendeleo ya mtoto. Hisia huathiri namna anavyojitambua, kuhusiana na wengine na kukabiliana na changamoto za maisha. Watoto hupitia hisia mbalimbali kama furaha, huzuni, hofu, hasira, upweke, matumaini na upendo kulingana na mazingira wanamoishi. Kulingana na Nikolajeva (2013), hisia hizo zinaweza kusawiriwa kwenye matini ya watoto ili kuwasaidia wasomaji kuelewa mitazamo ya watu wengine. Ukuaji mzuri wa kihisia humwezesha mtoto kutambua hisia zake, kuzieleza kwa namna inayofaa na kuzidhibiti bila kujidhuru wala kuwaumiza wengine.

Kumschick et al. (2014) walitumia muundo wa kimajaribio wenye kundi la utafiti lililodhibitiwa kupima mabadiliko ya umahiri wa kihisia baada ya programu ya fasihi. Utafiti wao ulionyesha kuwa fasihi inaweza kukuza uwezo wa mtoto wa kuelewa hisia. Watoto waliosoma na kujadili fasihi walikuza umahiri wa kihisia. Walithibitisha kwamba fasihi iliyosomwa na kujadiliwa iliweza kusaidia watoto kuongeza maarifa na msamiati wa hisia. Utafiti wao ukipendekeza tafiti zaidi zifanywe kwa kutumia fasihi za lugha mbalimbali. Utafiti wao ulichunguza tu fasihi ya Kiingereza. Kadhalika utafiti wao haukuchunguza maudhui ya familia na athari zake kwa hisia za watoto. Mtafiti akitumia vitabu vya Kiswahili kubaini iwapo msamiati wa hisia umetumiwa. Aidha, makala haya yalishughulikia suala la familia kama chanzo cha hisia za watoto.

Tafiti kuhusu maendeleo ya mtoto zinaonyesha kuwa uwezo wa kutambua na kudhibiti hisia hujengwa hatua kwa hatua kupitia mwingiliano wa mtoto na familia, shule na jamii. Hivyo, mazingira yanayomzunguka mtoto huchangia kuimarisha au kudhoofisha ustawi wake wa kihisia. Nikolajeva (2013) alitumia msimamo unaooana na huu kusisitiza kuwa fasihi inaweza

kutumiwa kukuza uelewa wa hisia na huruma. Fasihi ya watoto huibua mazingira hayo kwa kuwasawiri watoto wanaopitia changamoto zinazofanana na zile zinazopatikana katika maisha halisi. Kwa njia hiyo, wasomaji hujifunza kutambua na kuelewa hisia mbalimbali.

Familia ndiyo mazingira ya kwanza ambayo mtoto hujifunza kujenga uhusiano na kuelewa hisia zake. Kwenye familia mtoto hupata mapenzi, ulinzi, mawasiliano na namna ya kushughulikia changamoto mbalimbali za maisha. Hata hivyo, changamoto kama kifo cha mzazi, talaka, migogoro ya kifamilia, kupuuzwa na kutengwa huathiri ustawi wa kihisia wa watoto.

Katiba ya Kenya (2010) pamoja na Sheria ya Watoto (2022) inatambua wajibu wa wazazi katika kulinda maslahi bora ya mtoto. Ingawa sheria hizi hazizungumzi hisia za mtoto kama kipengele kilichojitegemea; ulinzi wa maendeleo ya kimwili, kiakili, kijamii na kisaikolojia unahusisha ustawi wa kihisia. Hivyo basi, mtoto anayekulia katika mazingira yenye migogoro ya kifamilia huwa katika hatari ya kupata athari zinazoweza kuathiri ukuaji wake wa jumla.

Kutokana na hali hiyo, waandishi wa fasihi ya watoto wameanza kuwasawiri watoto wanaokabiliana na changamoto mbalimbali za kifamilia. Usawiri huo unawiana na uhalisia wa jamii ya kisasa. Usawiri huo huonyesha kuwa hisia za watoto si za kupuuzwa bali ni sehemu muhimu ya kuelewa maisha yao.

Miongoni mwa dhima muhimu za fasihi ya watoto ni kuwasaidia wasomaji kuelewa hisia zao na za wengine. Ngugi (2015) anaeleza kuwa fasihi inaweza kutumiwa kama bibliotherapia. Kwa njia hii fasihi huwawezesha watoto kujitambua kupitia tajriba za wahusika wanaokabili changamoto zinazofanana na zao. Kupitia usomaji, watoto hupata nafasi ya kutafakari hisia zao, kutambua kuwa hawako peke yao na kujifunza njia salama za kukabiliana na changamoto mbalimbali.

Aidha, fasihi ya watoto huchangia kukuza huruma, ustahimilivu na uwezo wa kujenga uhusiano bora. Wahusika wanaopitia changamoto za kifamilia huwapa wasomaji nafasi ya kuelewa kuwa hisia kama huzuni, hofu, hasira au upweke ni sehemu ya maisha ya binadamu na zinaweza kushughulikiwa kwa msaada wa familia, marafiki na jamii. Kwa mtazamo huu, fasihi ya watoto inakuwa nyenzo muhimu ya elimu ya kijamii na kihisia kwa kuwa inachangia kukuza uwezo wa watoto kutambua, kueleza na kudhibiti hisia zao.

Msingi wa Kinadharia

Makala haya yaliongozwa na Nadharia ya Uhalisia. Nadharia hii husisitiza uwakilishi wa maisha ya binadamu jinsi yalivyo, bila kupotosha ukweli wa tajriba za kijamii na kihisia. Tangu kuibuka kwake nadharia hii imekuwa msingi muhimu wa kuchunguza fasihi. Imeeleza jinsi fasihi inavyoakisi maisha ya jamii, migongano yake na changamoto zinazowakabili wanadamu. Kwa mtazamo huu, fasihi haipaswi kuonyesha ulimwengu wa kufikirika pekee, bali pia kuibua hali halisi zinazowagusa watu katika maisha yao ya kila siku. Miongoni mwa wanafalsafa waliochangia msingi wa nadharia hii ni Hegel (1971), ambaye alisisitiza kuwa sanaa na kielelezo cha uhalisia wa maisha ya jamii na maendeleo ya fikra za binadamu. Kulingana na Hegel (1971), fasihi hupata thamani ikionyesha ukweli wa maisha ya mwanadamu. Matukio na tajriba za watoto katika fasihi haziwezi kutenganishwa na mazingira ya familia na jamii wanamoishi. Mazingira hayo huunda sehemu kubwa ya ulimwengu wao wa kihisia.

Mawazo ya Scheilling (1989), yanakamilisha mtazamo huo kwa kusisitiza kuwa sanaa huibua ukweli. Ukweli huo hauwezi kufafanuliwa kikamilifu kwa mantiki ya kawaida. Kupitia wahusika, migogoro na tajriba zao, fasihi hufichua maisha ya ndani ya mwanadamu. Maisha hayo huonyesha mawazo, hisia na matumaini yao. Katika fasihi ya watoto, mtazamo huu unaonyesha kuwa hisia za mtoto si matokeo ya matukio tu, bali uzoefu wa ndani unaojengwa na mazingira yake.

Kwa upande mwingine, Flaubert (1963), alisisitiza waandishi wawasilishe maisha kwa uaminifu bila kupamba wala kuficha ukweli wake. Kwa mtazamo huo fasihi ni kioo cha jamii. Waandishi huonyesha maisha ya watu pamoja na changamoto wanazokabiliana nazo. Mifano ni kama usawiri wa watoto wanaopitia kifo cha mzazi, migogoro ya kifamilia, unyanyasaji wa kihisia, umasikini, kutengwa na changamoto za utambulisho. Matukio haya huwasilisha maisha halisi ya watoto wala si visa vya

kubuni vya burudani pekee. Waandishi wanaoegemea uhalisia, huwachora watoto wanaotambua, kueleza na kukabiliana na hisia zinazotokana na changamoto za maisha yao. Kwa kufanya hivyo, fasihi humwezesha msomaji kuelewa kuwa hisia ni sehemu ya maisha ya kawaida ya mtoto. Kulingana na makala haya fasihi ya watoto ni kioo cha ulimwengu wao wa kihisia. Kulingana na utafiti huu, watoto si wahusika wa pembeni wanaopokea maamuzi ya watu wazima pekee, bali wanaweza kupitia na kueleza hisia zao changamano.

Utafiti huu ulitumia mihimili ifuatayo: Fasihi huakisi hali halisi ya jamii. Mhimili huu ulitumika kuchunguza iwapo novela inaakisi changamoto zinazoweza kutokea katika maisha halisi. Changamoto hizo ni kama vile kifo na migogoro ya kifamilia. Utafiti ulibaini uwepo wa changamoto hizo na athari zake kwenye hisia za watoto.

Mhimili wa pili ni kwamba matendo ya wahusika huchochewa na mazingira yao ya kijamii na hali ya kisaikolojia. Kulingana na mhimili huu, hisia za wahusika watoto huathiriwa na mazingira ambayo wanaishi. Mazingira haya yanaweza kuwa umaskini, kifo, talaka na migogoro ya familia.

Mhimili wa tatu ni kwamba fasihi huwasilisha ukweli wa maisha bila kupotosha uhalisia. Flaubert (1963) anahimiza usawiri unaoonyesha uaminifu bila kuficha ukweli wa maisha. Hivyo basi, utafiti ulichunguza jinsi watoto walivyoeleza hisia zao bila kuficha ukweli uliochangia hali zao.

MBINU ZA UTAFITI

Makala haya yalitumia muundo wa kimaelezo ili kufafanua kuhusu uwasilishaji wa hisia za watoto kwenye fasihi. Data iliyotumiwa kwenye makala haya ilikusanywa baada ya kusoma makala mbalimbali kuhusu fasihi ya watoto, familia, malezi na hali za kihisia za watoto. Utafiti huu ulifanyiwa maktabani. Aidha, makala haya yalitumia novela tatu kama sampuli lengwa: novela hizo ni pamoja na *Ahaa! Roda* cha Tom Nyambeka (2017), *Mshale wa Matumaini* cha John Habwe (2022) na *Siri ya Baba Yangu* cha Yahya Mutuku (2017). Novela hizi ziliteuliwa kimakusudi kwani wahusika wakuu na wasimulizi ni watoto ambao walidhihirisha hisia hizo waziwazi. Aidha, suala la familia lilijitokeza tangu mwanzo hadi mwisho wa hadithi. Makala haya yanatambua kuwa hisia mbalimbali zilidhihirika katika simulizi, ila yalishughulikia tu zile zilizohusisha masuala ya familia. Uteuzi wa data ulilenga sehemu na matukio yaliyodhihirisha hisia zilizotokana na familia na mazingira yake. Data ilifasiriwa kwa kutumia nadharia ya uhalisia.

MATOKEO YA UTAFITI

Fasihi ya Watoto kama Nyenzo ya Kukuza Uelewa wa Hisia

Uchanganuzi wa novela *Ahaa! Roda* (Nyambeka, 2017), *Siri ya Baba Yangu* (Mutuku, 2017) na *Mshale wa Matumaini* (Habwe, 2022) unaonyesha kuwa fasihi ya watoto si chombo cha burudani na kufunza maadili tu, bali ni nyenzo muhimu ya kukuza uelewa wa hisia za watoto. Watoto waliosawiriwa walionyesha hisia zao. Isitoshe, walihoji chanzo cha hali zao. Walitambua, wakatafakari, wakadhibiti na wakaeleza hisia zao. Waandishi waliwajenga kwa njia iliyowezesha msomaji kuelewa kuwa hisia za watoto ni sehemu halisi ya maisha yao. Maelezo haya yakiunga mkono Bakize (2014) na Wamitila (2010) kuwa fasihi ya watoto husawiri ulimwengu wa mtoto. Hisia ni ulimwengu wa ndani wa mtoto.

Novela teule, zilihalalisha hisia za watoto. Waandishi wa novela hizo walionyesha kuwa watoto huathiriwa kihisia kwa kiwango kinacholingana na watu wazima. Katika *Ahaa! Roda*, Roda alionyesha huzuni, hofu na upweke baada ya kupoteza wazazi. Mwandishi akitumia hisia hizo kuonyesha pengo linaloachwa wazazi wakifariki. Vilevile, hisia hizo zinaonyesha mtoto aliyepoteza msingi wa usalama na mapenzi.

> *Hali hii ilikuwa imemwathiri Roda sana. Tulipokuwa skulini kila wakati angalionekana amejikunyata na kushika tama huku msongo ukiivamia na kuidunga nafsi yake... Alikuwa ameupoteza udamisi kabisa... (Ahaa! Roda Uk. 22).*

Vivyo hivyo, katika *Mshale wa Matumaini*, Zingo alipitia mgogoro mkubwa wa kihisia baada ya familia yake kusambaratishwa na ghasia za kikabila. Katika *Siri ya Baba Yangu* Fadhili aliishi katika upweke na majeraha ya kihisia licha ya kukua katika mazingira ya ukwasi wa mali. Mifano hiyo ikionyesha hali mbalimbali ambazo

huzua hisia katika maisha ya watoto. Aidha, waandishi wa novela waliwachora wahusika walioeleza hisia zao kwa uwazi. Kutumia watoto kama wahusika wakuu na wasimulizi kuliwapa nafasi ya kusimulia tajriba zao wenyewe. Usawiri wa tajriba za wahusika unaweza kuwa funzo kwa watoto wasomaji (Bakize ,2014).

Kupitia simulizi zao, hisia kama huzuni, hofu, upweke, hasira, kukataliwa, matumaini na furaha zinajitokeza waziwazi. Msamiati huu unaorejelea hisia ukidhibitisha kuwa matumizi ya msamiati wa hisia katika fasihi ya watoto ni njia mmoja ya kukuza uelewa wa kihisia (Kumschick et al., 2014). Usawiri huu ukitumia nadharia ya uhalisia kuonyesha kuwa hisia hutokana na tukio ambalo linaweza kutokea katika jamii. Kwa hivyo, fasihi huwasaidia watoto kutambua hisia hizo, kuzitofautisha na kuelewa mazingira yanayoweza kuzizalisha. Uwezo huu wa kutambua, kueleza na kudhibiti hisia ni msingi muhimu katika saikolojia ya mtoto, (Nikolajeva, 2013).

Fasihi pia hujenga huruma na uwezo wa kuona dunia kupitia macho ya wengine. Mwandishi wa Ahaa! Roda alimtumia Fadhili kama rafiki aliyemwelewa na kumfaa Roda wakati wa majonzi. Fadhili alishuhudia maumivu ya Roda na akajifunza kutazama changamoto zake kwa kumuelewa wala si kumhukumu.

> *Siku zote nilikaa naye karibukaribu kama pua na mdomo angaa kumshauri na kumtuliza... (Ahaa! Roda Uk. 22).*

Kwa msingi huo, fasihi hupanua uwezo wa mtoto kutambua kuwa watu wanaweza kuonyesha tabia tofauti kutokana na majeraha ya kihisia wanayoyabeba. Hivyo basi, fasihi ya watoto huchangia kujenga jamii yenye huruma , inayotambua na kuheshimu hisia za wengine.

Makala pia, yalibaini kuwa matumizi ya hisia hasi ni njia ya kihalisia ya kuakisi namna watoto wanavyokabiliana na changamoto. Changamoto za maisha halisi hazihusishwi kwa lengo la kuwakatisha tamaa. Badala yake, hisia hizo hutumiwa kujenga matumaini na ustahimilivu. Wahusika wakuu walikumbana na changamoto kubwa za kifamilia. Lakini wengi wao walipata watu au mazingira yaliyowasaidia kuendelea na maisha. Katika *Ahaa! Roda*, msaada wa rafikiye Fadhili na Ami yake Bw. Kilemba Roda ulimsaidia kuendelea licha ya misukosuko aliyopitia.

Katika *Mshale wa Matumaini*, Zingo alipata wosia na urafiki kutoka kwa Mzee Musambale ambaye alikuwa nguzo muhimu ya kurejesha matumaini yake.

> *Sawa Zingo lakini lazima usome kwa bidii ndipo ufaulu kufanya hivyo. Tunaendelea kukutafutia msaada katika mataifa ya ughaibuni, Mzee Musambale alisema kwa msisitizo fulani (Mshale wa Matumaini Uk. 51).*

Vivyo hivyo, Fadhili katika *Siri ya Baba Yangu* alipata faraja na urafiki kutoka kwa Mateso. Isitoshe, mwazo yalipomzidia angezungumza na msiri na dereva wake Mzee Kautipe. Kwa mtazamo wa kihalisia, fasihi ya watoto huwasilisha changamoto na suluhisho ambazo zinapatikana katika jamii. Changamoto hizo huibuliwa na mazingira yao na zinaonyesha athari halisia ya kihisia.

Kifo cha Mzazi na Athari Zake kwa Ustawi wa Kihisia wa Mtoto

Uchanganuzi wa novela teule ulisawiri kifo cha mzazi kama mojawapo ya changamoto za kifamilia. Kifo ni tukio la kihalisia ambalo huwa katika maisha ya binadamu. Kifo husababisha athari kubwa katika ustawi wa kihisia wa watoto. Katika *Ahaa! Roda* na *Mshale wa Matumaini,* waandishi walisawiri kifo cha mzazi kama tukio la mwisho wa maisha. Mwisho huo ukawa mwanzo wa mabadiliko katika ulimwengu wa kihisia, kijamii na kimaendeleo wa mtoto. Kwa mtazamo huu, fasihi ya watoto iliweka wazi kuwa majonzi ya mtoto hayaishii siku ya mazishi. Majonzi huendelea kuathiri namna mtoto anavyojiona na kuhusiana na wengine. Katika *Ahaa! Roda*, kifo cha Bw. Gidamu kilikuwa chanzo cha migogoro iliyobadili maisha ya Roda. Yeye hakupata ulinzi na faraja baada ya kumpoteza baba yake. Alikumbana na changamoto kama tamaa ya mali, kutekwa nyara, kunyimwa haki zake na hatimaye kumpoteza mama yake pia.

> *Kitendo hicho kilikuwa kimewatonesha wanakijiji kidonda ambacho kilikuwa bado kupona. Ni miezi michache tu iliyopita baada ya babake Roda kufa!*

> *Iweje mtu mwenye akili razini kumtesa kiokote kama huyu? (Ahaa Roda uk 13).*

Mwandishi alionyesha kuwa athari za kifo cha mzazi ziliibua unyonyaji, ukatili na kutengwa. Mwandishi aliakisi watoto wanaopoteza si mzazi tu bali pia usalama na uthabiti wa maisha.

Vivyo hivyo, katika *Mshale wa Matumaini*, Zingo alishuhudia kusambaratika kwa familia yake kutokana na ghasia za ukabila. Kupotea kwa baba yake na baadaye kifo cha mama yake. Mambo haya yalimwachia upweke na sintofahamu kuhusu maisha yajayo. Hisia zilimzidia alipohusishwa na matendo ya baba yake. Jambo hilo lililomfanya ajione mwenye hatia kwa kosa ambalo hakulifanya. Kwa njia hii, fasihi inaonyesha kuwa athari za msiba huweza kuongezwa au kupunguzwa na maoni ya jamii inayomzunguka mtoto.

Mbali na huzuni, novela hizi zilionyesha kuwa kifo kiliathiri maendeleo mengine ya mtoto. Roda alianza kudorora shuleni kutokana na msongo wa mawazo na ukosefu wa mazingira salama. Vivyo hivyo, Zingo alikabiliwa na changamoto masomoni. Isitoshe, alilemewa kujenga uhusiano kwani alihusishwa na makosa ya babake. Matokeo haya yakionyesha kuwa ustawi wa kihisia na maendeleo ya elimu haviwezi kutenganishwa. Mtoto anayekosa utulivu wa kihisia mara nyingi hupata ugumu wa kujifunza na kushirikiana na wengine.

> *Siku niliziona ndefu kuliko kawaida. Sikuwa na marafiki wengi wa kuchezea nao. Nilishinda pweke. Nilihuzunika na hali hiyo ya huzuni na majonzi... Mawazo ya kuacha shule yalikuwa yakinirudiarudia kila siku (Mshale wa Matumaini, Uk 43).*

Usawiri huu ukiunga mkono utafiti wa Arruda- Colli et al. (2017) ambao walitafiti usawiri wa kifo katika fasihi na kutambua kuwa huzuni ni mojawapo wa athari ambazo hujitokeza baada ya kufiwa na mzazi. Kulingana nao fasihi ya watoto haiwafunzi tu kuhusu kifo bali athari za kihisia na kijamii ambazo huzuka kutokana na hali hii. Aidha walibaini kuwa vitabu vya fasihi viliwapa watoto njia salama za kukabiliana na athari za kihisia za kifo. Kazi yao ilishughulikia tu vitabu vya Kihispania, Kiingereza na Kifaransa. Makala haya yakitumia mifano ya kutoka fasihi ya Kiswahili kukamilisha maoni yao.

Kwa upande mwingine, waandishi hawakuacha watoto hawa katika hali ya kukata tamaa. Katika visa vyote, waandishi walisawiri wahusika waliowapa msaada wa kihisia, ushauri au ulinzi. Hivyo, fasihi inaonyesha kuwa ingawa kifo cha mzazi ni tukio lenye maumivu makubwa, uwepo wa watu wazima wanaojali waathiriwa hupunguza athari zake. Matokeo haya yanaafikiana na maandiko kuhusu bibliotherapia Ngugi (2015) yanayoonyesha kuwa hadithi zinaweza kuwasaidia watoto kuelewa na kukabiliana na huzuni kwa kuwaonyesha kuwa hisia zao ni za kawaida na kwamba wengine wamepitia hali kama hizo. Aidha, yanawiana na utafiti wa Hoppe et al. (2025) kuhusu maendeleo ya mtoto baada ya msiba. Kulingana naye jamii na familia inayomzunguka mtoto humsaidia kupunguza hisia za msiba. Usawiri wa kifo cha mzazi na wahusika wanaopata msaada wa kijamii ni wa kihalisia. Kwa hivyo, kifo cha mzazi si tukio la kuibua huruma tu, bali ni taa kuhusu mwelekeo mpya wa maisha ya mtoto.

Migogoro ya Kifamilia na Athari Zake kwa Hisia za Mtoto

Uchanganuzi wa novela teule ulionyesha kuwa migogoro ya kifamilia na kuvunjika kwa uhusiano ya wazazi husababisha majeraha ya kihisia kwa watoto. Waandishi wa *Ahaa! Roda* (Nyambeka, 2017), *Mshale wa Matumaini* (Habwe, 2022) na *Siri ya Baba Yangu* (Mutuku, 2017) walionyesha kuwa migogoro ya kifamilia haiathiri uhusiano wa watu wazima pekee. Migogoro hiyo humgusa mtoto na kubadili hali yake ya usalama, utambulisho, uhusiano na matarajio ya maisha. Kwa mtazamo huu, mtoto huathiriwa na migogoro ambayo hawezi kudhibiti.

Katika *Ahaa! Roda*, mgogoro wa urithi uliozuka baada ya kifo cha Bw. Gidamu. Tamaa ya mali ikavunja mshikamano wa familia na kuhatarisha maisha ya Roda. Roda alibakia kwenye hali ya hofu na ukatili. Badala ya ami Sumu kuwa nguzo kwa Roda, aligeuka kuwa chanzo cha mateso. Mtu aliyefaa kutegemewa na mtoto ndiye aliyeibua hisia za kutengwa, na hofu ya maisha. Mwandishi alionyesha kuwa migogoro ya kifamilia ilibebesha mtoto mizigo ya kihisia.

> *Baada ya Roda kurejelewa na fahamu, wanakijiji walianza kumdadisi na kumsaili jinsi hali ilivyokuwa wakati ule wa kutekwa nyara. Roda alielezea kwa ufasaha jinsi alivyotekwa nyara. Kumbukizi zake zilikuwa nzuri. Sote tulishangaa alipomtaja ami yake Sumu kuwa mmoja kati ya wale waliotaka kumfisha. Machozi yalimdondoka ndondondo alipomsimulia jinsi ami yake alivyokuwa akimtolea vitisho vya kumwua (Uk.17).*

Katika *Mshale wa Matumaini*, migogoro ya kikabila ilisababisha kusambaratika kwa uhusiano ya wazazi. Babake Zingo alishiriki katika vitendo vya ghasia. Familia yake ilipoteza mshikamano wake. Zingo alilazimika kukabiliana na mgongano kati ya kumpenda baba na kuchukia matendo yake.

> *Nilitamani kuuvua uhusiano na baba yangu. Nilisikitika sana. Nilijichukia (Mshale wa Matumaini uk.40).*

Mgongano huu ulizua mgogoro wa utambulisho. Zingo alihoji nafasi yake kuhusu utambulisho wake, alitamani kutonasibishwa na makabila ya wazazi wake. Mwandishi alionyesha hofu ya mtoto aliyekosa utambulisho katika jamii.

Katika *Siri ya Baba Yangu*, mgogoro ulisababishwa na ukosefu mawasiliano na ukaribu wa kihisia kati ya baba na mwana. Fadhili alikulia katika nyumba yenye utajiri mkubwa wa mali lakini yenye umaskini wa mawasiliano, mapenzi na furaha. Baba yake alishindwa kujenga uhusiano wa karibu naye. Mara nyingi alitumia mamlaka, vitisho na adhabu kama msingi wa malezi. Matokeo yake ni kwamba Fadhili alianza kuiona nyumba yao kama jehanamu badala ya mahali pa usalama. Usawiri huu ukionyesha kuwa hata familia isiyokumbwa na umaskini inaweza kumwachia mtoto majeraha ya kihisia iwapo urafiki utavunjika.

Watoto wanaokulia katika mazingira ya migogoro huanza kuhoji thamani yao, nafasi yao katika familia. Wengine hukosa thamani ya maisha na uwezo wao wa kuamini watu wengine. Waandishi walisisitiza umuhimu wa kuwepo kwa watu wanaoweza kurejesha matumaini ya mtoto. Katika novela teule, walimu, marafiki, baadhi ya familia na wanajamii walijitokeza kama vyanzo vya msaada wa kihisia kwa mtoto. Msaada huo ulijenga upya imani yake kwa wengine.

Matokeo haya yanaafikiana na utafiti wa Auersperg et al. (2019) uliobaini kuwa talaka za wazazi ziliongeza mfadhaiko miongoni mwa watoto na ziliathiri hisia za watoto walioishi katika migogoro hiyo. Utafiti unasisitiza kuwa uhusiano salama ndani ya familia ni msingi wa ukuaji mzuri wa kihisia. Makala yakionyesha kuwa migogoro ya wazazi huongeza hatari kwa mtoto. Mtoto hupata wasiwasi, huzuni, matatizo ya kitabia na changamoto za kujenga uhusiano.

Kukataliwa na Mzazi: Usawiri Wake katika Fasihi ya Watoto

Matokeo ya uchanganuzi yalionyesha kuwa unyanyasaji wa kihisia ni mojawapo ya changamoto inayowakumba watoto. Unyanyasaji wa kimwili huacha majeraha yanayoonekana lakini unyanyasaji wa kihisia hujidhihirisha kupitia kukataliwa, kupuuzwa, kukosa mapenzi, kutishiwa, matusi, na ukosefu wa mawasiliano kati ya mtoto na mlezi. Mwandishi wa *Siri ya Baba Yangu* (Mutuku, 2017) alionyesha kuwa majeraha haya huathiri ukuaji wa kihisia, kijamii na saikolojia ya mtoto. Rohner et al. (2005) walieleza kuwa kukataliwa na mzazi huthibitishwa na tabia kama vile ukosefu wa mapenzi, ukali wa mzazi, mtoto kutosikilizwa na mtoto kupuuzwa. Mtoto anayepitia hali kama hii huwa na hofu na kutojiamini. Aidha, tabia na masomo yake yanaweza kuathirika. Hali kama hii imedhihirishwa na usawiri wa Fadhili katika *Siri ya Baba Yangu.*

Katika *Siri ya Baba Yangu*, Fadhili alikulia katika mazingira yenye utajiri wa mali lakini yenye upungufu wa kihisia. Baba yake alitimiza mahitaji ya kimwili lakini hakujenga uhusiano ambao ungeonyesha mtoto mapenzi. Fadhili alionyesha hisia za kutopendwa, kutosikizwa na kuthaminiwa.

> *Baba kumchukia mwana ukomo wa kumchukia ... Nilishangaa. Baba yangu hakuificha chuki yake dhidi yangu. Tangu nilipomjua kuwa baba yangu, hakunionyesha mapenzi yoyote yale (Siri ya Baba Yangu uk. 77).*

Mawasiliano kati yao yalitawaliwa na vitisho, ukimya na mamlaka badala ya upendo na ushauri. Kutokana na hali hiyo, Fadhili aliiona nyumba yao kama mahali pa mateso badala ya usalama. Utafiti huu ulikubaliana na maoni ya Mbithi (2019) kwamba baadhi ya wazazi waliwatelekeza watoto wao kwa kutowatimizia mahitaji yao ya msingi. Mojawapo ya mahitaji haya ya kimsingi ni mapenzi. Aidha, alieleza kuwa baadhi ya wazazi walikuwa na tabia zilizowaathiri watoto kisaikolojia na kihisia.

Usawiri huu ukionyesha kuwa mahitaji ya kihisia ya mtoto yana uzito uliolingana na mahitaji yake ya kimwili. Baadhi ya watoto hutafuta faraja nje ya familia. Fadhili alimwona Mateso na dereva wao kama watu wa kuaminika kuliko baba yake. Matokeo haya yakiendana na Sheria ya Watoto ya Kenya ya mwaka 2022. Mtoto anafaa kulindwa dhidi ya aina zote za unyanyasaji au mazingira yanayodhoofisha maendeleo yake.

Ustahimilivu wa Kihisia wa Watoto

Watoto wanaokumbwa na changamoto za kifamilia hupata fursa ya kujenga upya matumaini kupitia urafiki na wanajamii wanaowajali. Waandishi wa *Ahaa! Roda* (Nyambeka, 2017), *Mshale wa Matumaini* (Habwe, 2022) na *Siri ya Baba Yangu* (Mutuku, 2017) walionyesha kuwa uhusiano mbadala unaweza kuwa kinga dhidi ya athari za majeraha ya kihisia. Hivyo, fasihi ya watoto haisawiri mtoto kama mtoto asiye na matumaini, bali kama mhusika mwenye uwezo wa kujenga ustahimilivu anapopata msaada unaofaa.

Katika *Siri ya Baba Yangu*, Fadhili alikosa ukaribu wa kihisia kutoka kwa baba yake, lakini alipata faraja kupitia urafiki wake na Mateso. Urafiki huu ulimwezesha kueleza mawazo na hisia ambazo hangeweza kueleza wala kuonyesha nyumbani. Aidha, dereva wao, mzee Kautipe alikuwa mtu aliyemsikiliza na kumwelewa bila kumhukumu. Mwandishi alionyesha kuwa wakati mwingine mtoto hupata usalama wa kihisia kutoka kwa watu ambao si wazazi wao. Watu hawa huwa tayari kusikiliza, kuelewa na kukubali. Hali hii inasisitiza umuhimu wa kuwa na mtu mzima anayepatikana kwa ajili ya mtoto katika kipindi cha changamoto.

Katika *Mshale wa Matumaini*, masomo, kandanda na ushauri wa mzee Musambale unajitokeza kama nguzo muhimu za kurejesha matumaini ya Zingo. Licha ya kupoteza wazazi na kupitia maumivu ya ghasia za kikabila, elimu ilibaki kuwa matumaini yake. Jioni angecheza kandanda ili kupunguza mawazo. Mtoto anaweza kushiriki kwenye mambo ambayo yanamkumbusha kuwa bado ana nafasi ya kukubalika katika jamii.

Katika *Ahaa! Roda*, licha ya vipindi vya mateso na kutengwa, Roda alikutana na watu waliomwonyesha huruma na kumsaidia kurejesha imani yake kwa wengine. Alipata msaada na urafiki kutoka kwa Fadhili na Bw. Kilemba. Alirudi shuleni na akahitimu baada ya kurejewa na amani. Kwa hivyo, utafiti ulibaini kuwa ni wajibu wa jamii nzima kushughulikia maslahi ya mtoto. Uchambuzi unaonyesha kuwa urafiki uliojengwa katika novela hizo una sifa zilizochangia ustawi wa kihisia wa mtoto. Urafiki kwa watoto hutoa usikivu, faraja na kukubalika. Kupitia mazungumzo yao, watoto hupata nafasi ya kueleza hofu na matumaini yao.

Mchango wa Utafiti kwa Taaluma, Malezi na Sera

Makala haya yanatoa mchango kwa kuchunguza nafasi ya fasihi katika kukuza ustawi wa kihisia wa mtoto. Tafiti nyingi zimejikita katika masuala ya malezi, maadili na haki za watoto. Makala haya yameonyesha kuwa fasihi ya watoto inaweza kutumika kama nyenzo ya kuzitambua, kuzielewa na kuzijadili hisia za watoto. Matokeo yake yameonyesha kuwa uhalisia katika fasihi ya watoto unawasilisha ulimwengu wa ndani wa mtoto. Hisia, mawazo, hofu, matumaini na migogoro ya kihisia ni sehemu ya uhalisia unaopaswa kupewa uzito sawa na matukio ya nje. Makala haya yanaunga mkono sera zinazoendelezwa na Shirika la Afya Ulimwenguni WHO (2025) kuhusu ustawi wa na maendeleo ya kihisia miongoni mwa vijana. Utafiti wao ulithibitisha kuwa watoto huathiriwa na mazingira wanayokulia. Utafiti wao ulitaja mazingira kama vile familia. Aidha, makala yanaunga mkono kifungu cha 53 cha Katiba ya 2010 ambacho kinalinda maslahi ya mtoto kwa kuonya dhidi ya mambo yanayohatarisha ustawi wake.

Kwa upande wa elimu, makala haya yanaonyesha kuwa novela za watoto zinaweza kutumiwa kama nyenzo za kufundishia umahiri wa kijamii na kihisia pamoja na stadi za lugha. Walimu wanaweza kutumia visa na wahusika katika kuzua mijadala kuhusu hisia. Mbinu hii inaweza kuimarisha mazingira ya kujifunza

yanayomjengea mwanafunzi uwezo wa kujitambua, kueleza hisia zake kwa usalama na kuwaheshimu wengine.

Kwa upande wa malezi, matokeo yanasisitiza kuwa wazazi na walezi wanapaswa kutambua kwamba maendeleo ya mtoto hayapimwi kwa kutimizwa kwa mahitaji ya kimwili pekee. Upendo, mawasiliano, usikivu na uwepo wa mzazi ni nguzo muhimu za ustawi wa kihisia. Makala haya yanaonyesha kuwa watoto wanaolelewa katika mazingira yenye mawasiliano mazuri hujiamini kuliko wale wanaokulia katika mazingira ya hofu.

Kwa upande wa sera, matokeo yanaunga mkono juhudi za kuimarisha afya ya akili na ustawi wa watoto kupitia mfumo wa elimu na huduma za ulinzi wa mtoto. Makala haya yanapendekeza kuwa uteuzi wa vitabu vya watoto katika shule uzingatie pia uwezo wa kazi hizo kukuza afya ya kihisia, huruma na ustahimilivu, sambamba na kufundisha lugha na maadili.

Upungufu wa Utafiti

Makala haya yalijikita katika uchambuzi wa novela tatu. Hivyo, matokeo haya hayawezi kuwakilisha kwa ukamilifu fasihi yote ya watoto. Aidha, utafiti huu ulitumia uchambuzi wa matini pekee bila kukusanya maoni ya watoto wasomaji, walimu au wazazi kuhusu namna walivyopokea kazi hizi za fasihi. Kutokana na hali hiyo, baadhi ya tafsiri zinatokana na uchambuzi wa mtafiti na zinaweza kutofautiana na tajriba za wasomaji wengine.

HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

Hitimisho: Makala haya yalionyesha kuwa fasihi ya watoto imepanua upeo wake kutoka kuwa chombo cha burudani na mafunzo ya lugha hadi kuwa nyenzo muhimu ya kuakisi maisha halisi ya watoto. Kwa njia hii fasihi ya watoto inakuza ustawi wao wa kihisia. Kupitia uchambuzi wa Ahaa! Roda, Mshale wa Matumaini na Siri ya Baba Yangu, ilibainika kuwa waandishi waliwasilisha kwa uhalisia changamoto na athari zake kwa hisia za watoto. Aidha, makala haya yalionyesha kuwa pamoja na kusawiri majeraha ya kihisia, fasihi ya watoto imewasilisha mbinu za kukabiliana na hisia chanya. Kwa njia hii, fasihi ya watoto imetekeleza dhima ya bibliotherapia kwa kuwasaidia watoto kutambua hisia zao, kuzielewa na kujifunza mbinu salama za kukabiliana na changamoto za maisha.

Mapendekezo: Makala haya yanapendekeza tafiti zijazo zichunguze namna watoto wenyewe wanavyopokea na kufasiri hisia zinazowasilishwa katika fasihi ya watoto. Tafiti za aina hiyo zinaweza kutumia mbinu za mahojiano, vikundi jadili au uchunguzi darasani ili kubaini mchango halisi wa fasihi katika kukuza uelewa wa kihisia. Utafiti mwingine unaweza kuchunguza matumizi ya fasihi ya watoto katika kueneza ushauri nasaha na bibliotherapia katika shule za msingi na sekondari.

MAREJELEO

Arruda-Colli, M. N. F., Weaver, M. S., & Wiener, L. (2017). Communication about dying, death, and bereavement: A systematic review of children's literature. *Journal of Palliative Medicine, 20*(5), 548–559.

Auersperg, F., Vlasak, T., Ponocny, I., & Barth, A. (2019). Long-term effects of parental divorce on mental health: A systematic review and meta-analysis. *Journal of Psychiatric Research, 119*, 103–114.

Bakize, L. H. (2014). *Utangulizi wa fasihi ya watoto*. Moccony Printing Press.

Children Act, No. 29 of 2022 (Kenya).

Flaubert, G. (1963). On realism. In *Documents of modern literary realism*.

Habwe, J. (2022). *Mshale wa matumaini*. Access Publishers Ltd.

Hegel, G. W. F. (1971). *Introduction to aesthetics*. Clarendon Press.

Hoppe, R., Winter, M. A., Williams, C. D., & Sandler, I. (2025). When a parent dies: A scoping review of protective and risk processes for childhood bereavement. *Death Studies, 49*(5), 546–556. https://doi.org/10.1080/07481187.2024.2340729

Kumschick, I. R., Beck, L., Eid, M., Witte, G., Klann-Delius, G., Heuser, I., Steinlein, R., & Menninghaus, W. (2014). Reading and feeling: The effects of a literature-based intervention designed to increase emotional competence in second and third graders. *Frontiers in Psychology, 5*.

Lukens, R. J. (2007). *A critical handbook of children's literature* (8th ed.). Pearson Allyn and Bacon.

Mbithi, J. N. (2019). Single parenting in Kenya: Issues, challenges and solutions. *Mt. Kenya University Journal*.
Mutuku, Y. (2017). *Siri ya Baba yangu*. Queenex Publishers Limited.
Ngugi, P. M. (2015). Mbinu na mikakati ya kutumia fasihi ya watoto kama bibliotherapia. *Kioo cha Lugha*.
Nikolajeva, M. (2013). Picturebooks and emotional literacy. *The Reading Teacher,* 67(4), 249–254. https://doi.org/10.1002/trtr.1229
Nodelman, P. (2008). *The hidden adult: Defining children's literature*. Johns Hopkins University Press.
Nyaga, F. M. (2022). Itikadi za kisiasa katika fasihi ya watoto ya Kiswahili. *Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam*.
Nyambeka, T. (2017). *Ahaa! Roda*. Queenex Publishers Limited.
Republic of Kenya. (2010). *The New Kenyan Constitution*. Government Printers.
Rohner, R. P., Khaleque, A., & Cournoyer, D. E. (2005). Parental acceptance-rejection: Theory, methods, cross-cultural evidence, and implications. *Ethos, 33*(3), 299–334.
Scheilling, F. W. J. (1989). *The philosophy of art* (D. W. Stott, Trans.). University of Minnesota Press.
Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa fasihi: Misingi na vipengele vyake*. Phoenix Publisher Limited.
Wamitila, K. W. (2010). *Kanzi ya fasihi: Misingi na uchanganuzi wa fasihi*. Vide-Muwa Publishers Ltd.
World Health Organization. (2025). *Mental health of adolescents*. World Health Organization.